# Ulinganishi wa Kiisimu wa Lugha za Kiswahili na Kiarabu

*Zainab Ali Iddi*[1] na *Hamad Khamis Juma*[2]
[1]*Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar*
[2]*Chuo cha Ualimu Mazizini*

**Ikisiri**

**Makala haya yanalinganisha vipengele vya kiisimu baina ya lugha za Kiswahili na Kiarabu ili kubaini iwapo lugha hizi zina asili moja au la. Itakumbukwa kwamba mnamo mwanzoni mwa miaka ya 1970 katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam palijitokeza mijadala iliyozusha mabishano na malumbano ya kitaaluma kuhusu asili na chimbuko la lugha ya Kiswahili. Kuna waliodai kuwa lugha ya Kiswahili ilitokana na lugha ya Kiarabu na wengine wakaeleza kuwa Kiswahili ni lugha ya Kibantu (Massamba, 2007). Ushahidi wa kila upande uwe na mashiko au usiwe na mashiko ulitolewa, lakini ulinganishi wa kiisimu wa lugha hizi bado haujafanyika. Kwa sababu hiyo ndipo tukaamua kulinganisha isimu ya lugha mbili hizi. Data ya uchunguzi huu imekusanywa kutoka maktabani ambapo mwandishi amepitia maandiko na machapisho mbalimbali yanayohusiana na kazi hii. Matokeo ya uchunguzi huu yanabainisha kuwa lugha ya Kiswahili haitokani na Kiarabu. Kwa sababu katika vipengele vitano vya kiisimu tulivyovilinganisha katika makala haya, vyote vinaonesha kuwa lugha hizi zinatofautiana kiisimu. Vipengele vilivyolinganishwa ni msamiati wa msingi, fonolojia, mofolojia, sintaksia na mfumo wa ngeli. Kutokana na tofauti hizo tunaweza kuhitimisha kuwa lugha hizi hazina asili wala mnasaba mmoja.**

Maeno Muhimu: Kiswahili, Kiarabu, Isimu, Fonolojia, Mofolojia, Sintaksia, Mfumo wa Ngeli

**Utangulizi**

Kinyume na hapo awali ambapo Kiswahili kilikuwa ni lugha ya Upwa wa Afrika Mashariki, hivi sasa lugha hii imekuwa ikizungumzwa katika maeneo mengi ya Afrika ya Mashariki, Kati na Kusini. Katika wakati tulionao, Kiswahili ni lugha muhimu sana kwa mawasiliano ya wakazi wa Afrika Mashariki na kwingineko ulimwenguni (Massamba, 2007). Aidha, katika karne hii ya 21, Kiswahili kimekuwa lugha ya mawasiliano mapana zaidi hadi kusini mwa Afrika na Afrika kwa jumla. Hali hii inatudhirishia kwamba, Lugha ya Kiswahili imetokea kuwa na umuhimu mkubwa kuliko lugha nyingine za Kibantu; jambo ambalo linafanya pawe na umuhimu wa kuchunguza asili ya lugha hii.

Kwa mujibu wa Nurse (1982) mijadala ya historia ya Kiswahili, utamaduni na dini mara nyingi ilikuwa ikitawaliwa na mitazamo kwamba asili yake ni kutoka Mashariki ya Kati, Bara Hindi na Kusini Mashariki ya Asia. Kwa muda mrefu sana, kulikuwa na hali ya kutofautiana miongoni mwa wataalamu wa lugha na isimu kuhusu asili ya lugha ya Kiswahili. Kwa sababu kulikuwa na madai kwamba Kiswahili ni lugha iliyoingizwa katika upwa wa Afrika ya Mashariki na wageni wa Kiarabu kwa upande mmoja. Pia, kulikuwa na madai kuwa Kiswahili ni lugha yenye asili ya Kibantu yenye athari ya lugha nyingine kutokana na maingiliano ya ndani na nje ya bara la Afrika kwa upande mwingine (Massamba, 2002).

Nia ya makala haya si kujaribu kuchochea tena mijadala hiyo kwani ushahidi wa kihistoria, kiisimu na kiakiolojia umethibitisha dhahiri shahiri kuwa Kiswahili ni lugha ya Kibantu. Hata hivyo, ni muhimu kufanya ulinganishi wa vipengele vya kiisimu vya lugha mbili hizi ili kuweka bayana vipengele ambavyo kwa hakika ndivyo vilivyokuwa chanzo cha mtafaruku na msigano wa mawazo uliokuwepo kuhusu kadhia hii.

Aidha, madai kwamba Kiswahili asili yake ni Kiarabu yamekitwa katika kigezo cha wingi wa msamiati na dini ya kiislamu. Inadaiwa kwamba lugha ya Kiswahili ina msamiati mwingi wenye asili ya Kiarabu (taz. Polome 1967; Bosha 1993 na Lodhi 2000). Pia, inachukuliwa kwamba dini ya kiislamu katika upwa wa Afrika Mashariki ililetwa na Waarabu na kwa vile wakazi wengi wa pwani

ni waislamu basi Kiswahili nacho kililetwa na Waarabu (Massamba na wenzie, 2001). Hata hivyo, waumini wa mtazamo huu hawatuoneshi walau mfanano wa vipengele vya kiisimu baina ya lugha mbili hizi ili kuthibitisha madai yao.

Kama tulivyodokeza hapo awali kwamba lengo la makala haya ni kulinganisha na kujadili vipengele vya kiisimu baina ya lugha za Kiswahili na Kiarabu. Mjadala wa makala haya umezingatia vigezo vinavyotumiwa katika mbinu linganishi kama vile kuchunguza msamiati wa msingi, fonolojia, mofolojia, sintaksia na ngeli za nomino.

**Madai kwamba Kiswahili kinatokana na Kiarabu**

Kiswahili ni lugha ya Kibantu ambayo inazungumzwa katika maeneo ya Afrika Mashariki na maeneo mengine ulimwenguni ambapo Kiarabu ni lugha ya Kisemiti inayozongumzwa katika maeneo mbalimbali ya Bara Arabu na maeneo mengine ya ulimwengu (Akidah, 2013). Bila shaka zipo tafiti zilizokwishafanywa kulinganisha isimu ya lugha mbili hizi. Hata hivyo, kwa mujibu wa uelewa wetu hakuna uchunguzi wa kina ambao umefanywa kwa ajili hiyo. Hivyo basi, tumeshawishika kulinganisha vipengele vya kiisimu vya lugha mbili hizi ili kuweka bayana ukweli wa madai haya.

Kama tulivyosema hapo awali kuna baadhi ya wataalamu waliothubutu kudai kwamba lugha ya Kiswahili inatokana na lugha ya Kiarabu. Hata hivyo, mawazo yao yanakitwa kwenye msamiati na dini ya kiislamu. Ama bila shaka, hapa pana madai ya namna mbili; mosi, madai kwamba maneno mengi yenye asili ya Kiarabu yaliyomo katika Kiswahili yanaashiria kuwa lugha hii ilitokana na Kiarabu. Pili, inadaiwa kwamba kwa kuwa Kiswahili kilianza pwani na kwa kuwa idadi kubwa ya wenyeji wa pwani ni waislamu na kwa kuwa uislamu uliletwa na waarabu basi Kiswahili nacho kililetwa na Waarabu (Massamba na wenzie, 2001).

Ama kwa hakika, madai hayo yameshawahi kukanushwa na wataalamu kadhaa (k.m. Chiraghdin na Mnyampala (1977); Massamba na wenzie (2001); Massamba (2002, 2007)). Massamba na wenzie (2001) wanaeleza kwamba madai hayo hayana mashiko na yamekitwa katika vigezo ambavyo ni butu. Pamoja na ukweli usiopingika kwamba lugha ya Kiswahili imetokea kuwa na maneno mengi ya mkopo yenye asili ya Kiarabu, sababu hii haitoshi katika kuthibitisha madai yao. Hii ni kwa sababu wafanyabiashara kutoka Bara Arabu walikuwa na mawasiliano kwa karne nyingi zilizopita na wenyeji wa pwani ya Afrika Mashariki. Kama kwamba haitoshi, wageni hao kutoka Uarabuni walitamalaki na kutamakani katika maeneo mbalimbali ya mwambao wa Afrika ya Mashariki na visiwa vyake kwa muda mrefu. Kwa hiyo hapana shaka, wasemaji wa lugha mbili wanapokuwa na mawasiliano na mtagusano wa muda mrefu hawaachi kuathiriana.

Hata hivyo, tungependa kutanabahisha kwamba maneno ya mkopo katika lugha ya Kiswahili si kutoka lugha ya Kiarabu pekee. Pia, yamo maneno yenye asili ya Kiajemi, Kireno, Kijerumani, Kiingereza, hata lugha nyingine za Kibantu (Massamba na wenzie, 2001). Zaidi ya hayo, athari ya Kiarabu katika Kiswahili inaoneshwa kwenye kipengele cha msamiati tu ambapo msamiati huo siyo ule wa msingi. Pia, athari ya msamiati hiyo haihusu maumbo na miundo ya lugha. Uchunguzi mbalimbali uliokwishafanywa na watu kadhaa (Massamba, 2002, 2007) umedhihirisha kuwa Kiswahili ni lugha ya Kibantu kwa sababu wasemaji wake wengi ni Wabantu na lugha hii inafanana sana kiisimu na lugha za Kibantu.

Jambo la msingi na la kuzingatia ni kwamba kigezo cha lugha moja kuwa na maneno mengi ya mkopo kutoka lugha nyingine hakitoshi, hivyo basi kisichukuliwe kama sababu ya kueleza kuwa lugha hiyo inatokana na lugha nyingine. Kwa hakika, ni kawaida ya lugha nyingi ulimwenguni kukopa maneno kutoka lugha nyingine. Kwa mfano, lugha ya Kiingereza imechukua maneno mengi sana kutoka lugha ya Kifaransa. kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, Lugha ya Kiarabu nayo ina maneno mengi ya mkopo kutoka Kiingereza. Jambo muhimu la kuzingatia ni muundo wa lugha kifonolojia, kimofolojia, kimsamiati, na kisintaksia. Ikiwa lugha moja inafanana na nyingine katika vipengele hivyo vya kiisimu basi lugha hiyo inaweza kunasibishwa na nyingine.

Tukigeukia madai ya pili ambayo yananasibishwa na kigezo cha dini, kama wanavyosema Massamba na *wenzie* (2001), madai haya ndiyo mufilisi kabisa. Kwani, bila shaka, lugha na imani ni

vitu viwili faraka. Ikumbukwe kwamba lugha mbalimbali zimekuwepo ulimwenguni kabla ya majilio ya dini. Tuchukue mfano wa lugha ya Kiarabu, mathalani, imekuwepo ulimwenguni kwa karne nyingi kabla ya majilio ya dini ya Kiislamu. Ifahamike kwamba Uislamu ulipoingiya ulimwenguni uliwakuta wenyeji wakiwamo Waarabu wana lugha zao. Halikadhalika, lugha ya Kiingereza na lugha nyingine nyingi za Ulaya, Asia na Marekani, pia zimekuwepo kwa karne nyingi kabla ya majilio ya Ukristo (Massamba, 2002). Kwa mnasaba huo, lugha si kitambulisho cha imani ya mtu na wala imani si kitambulisho cha lugha ya mtu. Kwa maneno mengine, watu wa lugha moja wanaweza kuwa na imani tofautitofauti na kinyume chake. Tunachotaka kusisitiza hapa ni kwamba dhana hizi mbili zitofautishwe na kuwekwa bayana. Katika kuthibitisha kuwa utamaduni hauwezi kufungamanishwa na dini, Charaghdin na Mnyampala (1977) wanaeleza kwamba Uswahili haukuwa utamaduni wa Kiarabu kwa kufungamana na Uislamu bali utamaduni wa Kiswahili chimbuko lake ni mwambao wa Afrika ya Mashariki.

Kwa mintarafu hiyo, makala haya yanakusudia kuunga mkono hoja za akina Chiraghdin na Mnyampala (1997), Massamba na wenzie (2001) na Massamba (2002, 2007) zinazokanusha madai kwamba lugha ya Kiswahili inatokana na lugha ya Kiarabu. Hata hivyo, kwa upande wetu tumetumia kigezo kingine ambacho kinaunga mkono hoja hizo nacho ni kulinganisha vipengele vya kiisimu vya lugha mbili hizi na kuonesha tofauti zilizopo baina yake. Kabla hatujalinganisha litakuwa jambo la welekevu sana walau tukafafanua japo kwa muhutasari mkabala wa kinadharia ambao umetumika kuongoza uchambuzi wa data iliyotumika katika uandishi wa makala haya.

**Mkabala wa Kinadharia**

Kama tulivyodokeza hapo juu, madai kwamba Kiswahili kinatokana na lugha ya Kiarabu yamejadiliwa na kukanushwa na wataalamu mbalimbali wakiwemo Chiraghdin na Mnyampala (1977), Massamba (2002, 2007) na wengineo. Wataalamu hawa wametumia ushahidi wa kiisimu, kihistoria na wengine kiakiolojia kuthibitisha kuwa Kiswahili hakikutokana na Kiarabu. Kila mmoja ametumia mbinu yake kuthibitisha kwamba Kiswahili ni Kibantu. Massamba (2002, 2007), kwa mfano, anatumia *mbinu linganishi* kuthibitisha kuwa Kiswahili ni Kibantu. Katika ufafanuzi wake, Massamba (2007) anaeleza kuwa wanaisimu kwa kutumia mbinu hii hulinganisha lugha mbalimbali ili kuona kuwa lugha hizo zinatoka katika fuko moja au zinatoka katika fuko la lugha tofauti.

Hatahivyo, Ulinganishaji na mjadala wa vipengele vya kiisimu kuthibitisha kuwa lugha ya Kiswahili haikutokana na Kiarabu ambao ndio msingi wa makala haya, umezingatia mkabala wa kinadharia uliotumiwa na Anttila (1972) ujulikanao kama *mbinu linganishi.* Anttila aliitumia mbinu hii kulinganisha lugha za Kiswidi, Kiingereza na Kijerumani. Akifafanua mbinu hii Anttila (1972) anaeleza kuwa mbinu linganishi ni mbinu kuu inayotumiwa kuchambua lugha zaidi ya moja ambazo zina asili moja ili kuanzisha uhusiano wake wa kihistoria.

Kwa kutumia mbinu hii, tumeweza kulinganisha vipengele mbalimbali vya kiisimu kama vile msamiati wa msingi, fonolojia, mofolojia, sintaksia na ngeli za nomino baina ya lugha za Kiswahili na Kiarabu kama inavyobainishwa katika sehemu ifuatayo.

**Ulinganishaji wa Kiswahili na Kiarabu**

Katika kulinganisha lugha mbili au zaidi kwa madhumuni ya kutaka kuona iwapo lugha hizo zinatoka katika mame-lugha moja au la, mwanaisimu anapaswa kutumia vigezo vya isimu-linganishi (Anttila, 1972). Vigezo hivyo vimejadiliwa kwa kina na mifano kuntu kama inavyoonekana hapa chini.

**Mfumo wa Sauti**

Hiki ni kipengele kimojawapo cha msingi ambacho hutumiwa na wanaisimu ambapo hulinganisha sauti za lugha mbili au zaidi ili kuona iwapo lugha hizo zina sauti za aina moja (alfabeti) na mpangilio wa sauti katika lugha hizi zinafanana au zinatofautiana.

**Sauti za Kiswahili na Kiarabu**

Tukianza na sauti za lugha, Kiswahili kina vipandesauti 30 kati ya hivyo ni konsonanti 23, ambazo ni /p, b, m, f, v, θ, ð, t, d, n, ñ, s, z, l, r, ɟ, š, k, g, č, ŋ, ɣ, h/. Pia Kiswahili kina irabu 5 ambazo ni /i, ɛ, a, u, ɔ/ pamoja na nusu irabu 2 ambazo ni /w, y/ (Massamba na wenzie, 2004).

Kwa upande wa Kiarabu, lugha hii ina vipandesauti 34; konsonanti 26 nazo ni; /b, m, f, θ, ð, ðˤ, t, t̪ˤ , d, d̪ˤ, n, s, sˤ, z, l, r, dʒ, š, k, x, ɣ, q, ħ, ʕ, ʔ, h/. Kwa upande wa irabu ziko 6 ambapo miongoni mwao 3 ni ndefu na 3 fupi. Irabu 3 ndefu ni /i:, u:, a:/ na irabu 3 fupi ni /i, u, a/. Vile vile katika Kiarabu kuna na viyeyusho 2 navyo ni; /w, j/ (Akidah, 2013). Aidha, Katika lugha ya Kiarabu irabu fupi zinaweza kuwekwa au zisiwekwe kwenye konsonanti na maneno yakaweza kusomeka.

Kutokana na mifano hapo juu tunabaini kuwa kuna kutofautiana kwa sauti za lugha hizi mbili ambapo baadhi ya sauti zimekosekana na hazimo katika lugha ya Kiswahili lakini sauti hizo zinapatikana katika lugha ya Kiarabu nazo ni; /ðˤ, t̪ˤ, d̪ˤ, sˤ, q, ħ, ʕ, ʔ,/. Pili, kwa upande mwengine, pia baadhi ya sauti zilizomo katika lugha ya Kiswahili hazimo katika lugha ya Kiarabu, mfano /p, v, ñ, č, ŋ,/ na /ɛ, ɔ/. Muktadha huu unabainisha kuwa pamoja na kuwepo kwa mfanano wa sauti baina ya lugha hizi mbili lakini pia kuna kutofanana kwa baadhi ya sauti.

**Mchakato wa Uingiaji wa Maneno ya Mkopo**

Kama tulivyodokeza katika § 2.0, kuna madai kwamba Kiswahili kinatokana na Kiarabu. Madai haya yamekitwa katika kigezo cha maneno ya mkopo, ambapo Wanaoshikilia hoja hii hudai kuwa Kiswahili ni Kiarabu kwa sababu kina msamiati mwingi wenye asili ya Kiarabu. Kwa mujibu wa Mwita, (2009) maneno ya Kiswahili yanayodaiwa kuwa ya mkopo kutoka Kiarabu huingia katika lugha ya Kiswahili kwa njia ya utohozi. Maneno hayo yanapoingia kutoka lugha moja kwenda nyengine hupitia michakato mbalimbali. Miongoni mwa michakato hiyo ni uchopekaji wa irabu, ufupishaji wa irabu, udondoshaji wa konsonanti, ubadilishaji wa konsonanti, na michakato mingineyo. Hebu tuchunguze michakato hiyo na mifano hapa chini.

Kwanza, katika maneno mengi ya lugha ya Kiarabu yanapoingizwa katika Kiswahili hupitia mchakato wa *uchopekaji wa irabu.* Tuchunguze mifano ifuatayo:

| 1. | **Kiarabu** | | **Fonetiki** | | **Kiswahili** | **Tafsiri** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | /kibru/ | ⟶ | [kibr] | > | [kiburi] | ‘kiburi’ |
| | /mahru/ | ⟶ | [mahr] | > | [mahari] | ‘mahari’ |
| | /bardu/ | ⟶ | [bard] | > | [baridi] | ‘baridi’ |

Katika mifano (1) hapo juu tunabaini kuwa maneno yenye asili ya Kiarabu ambayo yana koda yanapoingizwa katika lugha ya Kiswahili huchopekwa irabu kuzuia silabi funge. Hii ni kwa sababu katika maneno ya Kiswahili kuna mashartizuizi yanayozuia silabi kuishia na koda.

Pili, katika lugha ya Kiswahili ni maneno machache yenye irabu ambazo hurefushwa. Lakini katika Kiarabu kuna maneno mengi sana ambayo yana irabu ndefu. Maneno hayo yanapoingizwa katika Kiswahili hupitia mchakato wa *ufupishaji wa irabu.* Tuangalie mifano ifuatayo:

| 2. | **Kiarabu** | | **Fonetiki** | | **Kiswahili** | **Tafsiri** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | /dali:lu/ | ⟶ | [dali:l] | > | [dalili] | ‘dalili’ |
| | /ka:tibu/ | ⟶ | [ka:tib] | > | [katibu] | ‘katibu’ |
| | /riba:u/ | ⟶ | [riba:] | > | [riba] | ‘riba’ |

Katika mifano (2) hapo juu tunabaini kuwa maneno yenye irabu ndefu kutoka lugha ya Kiarabu hupitia katika mchakato wa *ufupishaji wa irabu ndefu.* Mchakato huu huzuia urefushaji wa irabu kama ilivyo kama maneno mengi ya Kiswahili yanavyofuata mchakato huo.

Tatu, baadhi ya maneno ya lugha ya Kiarabu yana shadda wakati lugha ya Kiswahili haina shadda. Katika lugha ya Kiarabu, shadda ni mfuatano wa konsonanti mbili za aina moja ambazo hutamkwa

pacha kama konsonanti moja lakini kwa mkazo. Maneno ya Kiarabu yenye shadda yanapoingizwa katika Kiswahili hupitia mchakato wa *udondoshaji wa konsonanti*. Tuchunguze mifano hapa chini:

| 3. | **Kiarabu** | | **Fonetiki** | | **Kiswahili** | **Tafsiri** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | /šarru/ | → | [šarr] | > | [shari] | ‘shari’ |
| | /mahallu/ | → | [mahall] | > | [mahali] | ‘mahali’ |
| | /ħaððu/ | → | [ħaðð] | > | [ħaði] | ‘hadhi’ |

Katika mifano (3) hapo juu tunaona kuwa maneno ya lugha ya Kiarabu yenye shadda yanapoingizwa katika Kiswahili hudondosha konsonanti moja. Mchakato huu hufanyika ili kurahisisha matamshi ya maneno ambayo ni magumu kuyatamka.

Nne, katika § 4.1.1 tumedokeza kuwa kuna baadhi ya sauti za Kiswahili hazimo katika lugha ya Kiarabu na kinyume chake. Baadhi ya maneno hayo yanapoingizwa katika Kiswahili hupitia katika mchakato wa *ubadilishaji wa konsonati*. Tuangalie mifano ifuatayo:

| 4. | **Kiarabu** | | **Fonetiki** | | **Kiswahili** | **Tafsiri** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | /qabru/ | → | [qabr] | > | [kaburi] | ‘kaburi’ |
| | /baxtu/ | → | [baxt] | > | [bahati] | ‘bahati’ |
| | /ʔasˤlu/ | → | [ʔasˤl] | > | [asili] | ‘asili’ |

Kupitia mifano (4) hapo juu tunabaini kuwa maneno ya Kiarabu yenye konsonanti ambazo hazimo katika lugha ya Kiswahili basi konsonanti hizo hubadilika. Kwa mfano, /q/ > /k/, /x/ > /h/, /sˤ/ > /s/ na kadhalika. Mchakato huu hufanyika kuweka sauti mbadala ya ile inayokosekana katika Kiswahili.

Kwa ujumla, kupitia mifano (1)-(4) hapo juu tunabaini kuwa maneno ya Kiswahili ya mkopo yaliyoingia kutoka Kiarabu hayaingii katika Kiswahili yakiwa na uhalisia wake badala yake maneno hayo hutoholewa ili kufuata kanuni na taratibu za maneno ya lugha ya Kiswahili. Tukizingatia kwa makini tutabaini kuwa michakato yote tuliyoibanisha hapo juu inakusudia kurahisisha matamshi ya maneno ya Kiarabu katika Kiswahili. Pia, katika sehemu hii, tunaona tofauti za kifonolojia zilizopo baina ya lugha mbili hizi.

### Msamiati wa Msingi

Kuchunguza msamiati wa msingi ni kigezo kimojawapo kinachotumiwa na wanaisimu kulinganisha lugha mbili au zaidi katika kutafuta kuwepo kwa mnasaba wa lugha hizo. Massamba (2007) anafasili msamiati wa msingi kuwa ni aina ya msamiati ambao kwa kawaida huwa umetulia katika lugha. Msamiati huo hujumuisha vitu kama vile viungo vya mwili, hali za maumbile na vitendo vya maumbile ambavyo kwa kawaida havibadiliki kulingana na wakati au mitindo ya maisha. Kwa kutumia kigezo hiki, orodha ya maneno na maana zake kutoka lugha moja hulinganishwa na orodha ya maneno yenye maana zilezile kutoka lugha nyingine. Tuchunguze mfano ya viungo vya mwili hapa chini:

| 5. | **Kiswahili** | **Kiarabu** | | **Fonetiki** | **Tafsiri** |
|---|---|---|---|---|---|
| | jicho | /ʕainu/ | > | [ʕain] | ‘jicho’ |
| | uso | /wajhu/ | > | [wajh] | ‘uso’ |
| | ulimi | /lisa:nu/ | > | [lisa:n] | ‘ulimi’ |
| | kichwa | /ra’as/ | > | [ra’as] | ‘kichwa’ |
| | sikio | /uðn/ | > | [uðn] | ‘sikio’ |

Katika mifano (5) iliyobainishwa, ni dhahiri kwamba msamiati unaohusu viungo vya mwili siyo rahisi kubadilika katika lugha. Pia ni mara chache sana maneno ya kigeni kuchukua nafasi ya maneno hayo. Hii ina maana ya kusema kuwa msamiati wa msingi hauathiriwi na mabadiliko yanayoweza kusababishwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Aidha, mifano yetu inatuonesha kuwa kuna tofauti ya msamiati wa msingi baina ya Kiswahili na Kiarabu.

Vile vile, msamiati wa msingi hupatikana katika hali na vitu vya maumbile ambavyo havibadiliki katika mazingira ya kila siku. Tuchunguze mifano ifuatayo:

| 6. | **Kiswahili** | **Kiarabu** | | **Fonetiki** | **Tafsiri** |
|---|---|---|---|---|---|
| | jua | /shamsu/ | > | [shams] | 'jua' |
| | mwezi | /qamaru/ | > | [qamar] | 'mwezi' |
| | mbingu | /sama:wat/ | > | [sama:wat] | 'mbingu' |
| | ardhi | / arðˤ/ | > | [arðˤ] | 'ardhi' |
| | maji | /ma:u/ | > | [ma:u] | 'maji' |

Katika mifano (6) hapo juu tunabaini kuwa msamiati unaohusu vitu vya maumbile hauwezi kubadilika kutokana na wakati badala yake msamiati huu ni wa tangu na tangu. Hata hivyo, katika msamiati huo tunaona tofauti baina ya lugha mbili hizi kwani ni neno moja tu [ardhi] ambalo limefafana na Kiswahili. Bila shaka neno hili limeingia kwa njia ya mkopo kwa sababu neno hili limetoholewa kutoka katika Kiarabu [ardhw] kuwa [ardhi] katika Kiswahili.

Aidha, msamiati mwingine wa msingi ni vitendo vya maumbile ambavyo navyo huwa havibadiliki kulingana na mabadiliko ya jamii iwe ya kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kisayansi. Kwa kawaida kuna nguvu za maumbile zinazomfanya binadamu kutenda vitendo hivi. Tuangalie mifano ifuatayo:

| 7. | **Kiswahili** | **Kiarabu** | | **Fonetiki** | **Tafsiri** |
|---|---|---|---|---|---|
| | lala | /namu/ | > | [nam] | 'lala' |
| | simama | /qumu/ | > | [qum] | 'simama' |
| | fa | /mu:tu/ | > | [mu:t] | 'fa' |
| | cheka | /ðˤihak/ | > | [ðˤihak] | 'cheka' |
| | kohoa | /suʕa:l/ | > | [suʕa:l] | 'kohoa' |

Katika mifano (7) hapo juu tunabaini kuwa maumbo yote ya maneno ambayo yana maana sawa kati ya Kiswahili na Kiarabu yanatofautiana. Tulitarajia kwamba, kwa vile msamiati huu hutumiwa katika kila jamii ya binadamu, maumbo ya maneno hayo katika lugha hizi walau machache yafanane lakini hali imekuwa kinyume chake.

Kwa ufupi, katika mifano (5) – (7) hapo juu tunapata picha kuwa ama kwa hakika lugha hizi zinazonasibishwa kuwa na asili moja, kwa kiasi kikubwa sana zinatofautiana katika msamiati wa msingi. Pia, msamiati ambao utaingia katika lugha ya Kiswahili huingizwa baada ya kutoholewa ili kufuata kanuni na taratibu za lugha hii.

**Mfumo wa Maumbo ya Maneno**

Pia, katika kigezo cha mofolojia (mfumo wa maumbo ya maneno) maneno ya aina moja kutoka katika lugha zinazolinganishwa huchunguzwa ili kuona kuwa maneno hayo yana mfumo sawa au tofauti wa maumbo. Hebu tuchunguze mifano ya mfumo wa maumbo ya nomino kama ifuatavyo:-

| 8. | **Kiswahili** | **Kiarabu** | **Mofolojia** | **Tafsiri** |
|---|---|---|---|---|
| | ji-icho | ʕayn | ʕ-y-n | 'jicho' |
| | u-so | wajh | w-j-h | 'uso' |
| | u-limi | lisa:n | l-s-n | 'ulimi' |
| | ki-chwa | ra'as | r-'A-s | 'kichwa' |

Katika mifano (8) hapo juu tunabaini kwamba maneno katika orodha ya Kiswahili kila neno lina shina ambalo linatanguliwa na viambishi. Kwa kawaida viambishi hivi huitwa *viambishi awali au viambishi ngeli*. Lakini katika orodha ya maneno ya Kiarabu inayoonesha mofolojia ya maneno tunabaini kuwa kila neno linabakiwa na konsonanti ambazo zinasimama pekee. Kwa hiyo, tunabaini kuwa konsonanti hizi huchopekwa irabu ili kuunda maneno.

Baada ya kulinganisha maumbo ya nomino katika mifano (8) hapo juu, tunatumia kigezo hikihiki cha kimofolojia kulinganisha vitenzi vya Kiswahili na Kiarabu. Lengo ni kuona iwapo mfumo wa maumbo ya vitenzi vya lugha mbili hizi unafanana au unatofautiana. Tuangalie mifano hapa chini:

9.

| **Kiswahili** | **Kiarabu** | **Mofolojia** | **Tafsiri** |
|---|---|---|---|
| chek-a | dhwihak | dhw-h-k | 'cheka' |
| koho-a | suʕa:l | s-ʕ-l | 'kohoa' |
| lal-a | nam | n-m | 'lala' |
| simam-a | qum | q-m | 'simama' |
| f-a | mu:t | m-t | 'fa' |

Katika mifano (9) hapo juu tunabaini kuwa katika mfumo wa vitenzi vya lugha Kiswahili tulivyoviorodhesha, vinaanza na *mzizi* ambapo kila mzizi unafuatiwa na irabu [a] ambayo huitwa *irabu ishilizi*. Lakini katika vitenzi vya lugha ya Kiarabu tunabaini kuwa kila neno linabakiwa na konsonanti ambazo zinasimama peke yake. Konsonanti hizo ndizo ambazo huchopekwa irabu wakati wa kuunda maneno.

Kwa ujumla, katika mifano (8) na (9) hapo juu tunabaini kuwa kuna tofauti kubwa katika mfumo wa maumbo ya maneno (mofolojia) baina ya lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiarabu.

**Miundo ya Maneno**

Aidha, kigezo cha ulinganishi wa kisintaksia nacho kimetumika ili kulinganisha miundo ya tungo za lugha za Kiswahili na Kiarabu. Makala imebaini kuwa lugha ya Kiswahili inafuata mpangilio wa kiima-kitenzi-yambwa kinyume na lugha ya Kiarabu ambapo hutumia mpangilio wa kitenzi-kiima-yambwa kama inavyojibainisha katika mifano ifuatayo:

10.

| **Kiswahili** | **Kiarabu** |
|---|---|
| Mtoto anafua nguo | Yaghsilu twifilu almalaabisa |
| K KT YM | KT K YM |
| Mama anapika chakula | Tatwibakhu al'ummu twaʕamu |
| K KT YM | KT K YM |
| Msichana anambeba mtoto | Tahmilu bintu twifilun |
| K KT YM | KT K YM |
| Mvulana anasoma kitabu | Yaqrau swabiyyu kita:bun |
| K KT YM | KT K YM |
| Mwalimu anaandika barua | Yaktubul muʕalimu arisa:lat |
| K KT YM | KT K YM |

[K : Kiima, KT : Kitenzi, YM : Yambwa]

Katika mifano (10) hapo juu tunaona kuwa miundo ya tungo za Kiswahili inafuata mpangilio wa kiima-kitenzi-yambwa (K-KT-YM) lakini miundo ya tungo za Kiarabu inafuata mpangilio wa kitenzi-kiima-yambwa (KT-K-YM). Hii ndiyo mipangilio ya msingi kwa kila lugha japokuwa wakati mwingine Kiarabu kinaweza kufuata mpangalio wa kiima-kitenzi-yambwa ambao pia unakubalika licha ya kuwa sio mpangilio wa msingi. Tuangalie mifano ifuatayo:

11.

| **Kiarabu** | **Tafsiri** |
|---|---|
| Atwifilu yaghsilu almalaabisa | 'mtoto anafua nguo' |
| K KT YM | |
| Al'ummu tatwibakhu twaʕamu | 'mama anapika chakula' |
| K KT YM | |
| Almuʕalimu yaktubul arisa:lat | 'mwalimu anaandika barua' |
| K KT YM | |

12.**Kiswahili**

*Anafua mtoto nguo
KT K YM

*Anapika mama chakula
KT K YM

*Anaandika mwalimu barua
KT K YM

Katika mifano (11) hapo juu tunabaini kuwa katika lugha ya Kiarabu japokuwa mpangilio wa msingi wa tungo ni KT-K-YM lakini lugha hii inaweza pia kufuata mpangilio wa K-KT-YM ilhali tungo zake bado zinakubalika kisarufi. Lakini, katika mifano (12) hapo juu tunaona kuwa lugha ya Kiswahili inapobadili mpangilio wa msingi (K-KT-YM) tungo zake huwa na ukakasi wa kimatamshi kwa sababu ushikamani wa maneno katika mpangilio huu si wa kawaida. Hata hivyo, mpangilio huu mara chache hutumika katika lugha ya mazungumzo pale msemaji anapotaka kuonesha msisitizo.

Kwa muhutasari, katika mifano (10) hadi (12) hapo juu tunabaini kuwa mipangilio ya maneno katika lugha za Kiswahili na Kiarabu inatofautiana.

**Mfumo wa Uaninishaji wa Ngeli**

Tukigeukia kigezo cha mfumo wa ngeli za nomino, lugha ya Kiswahili inafuata utaratibu maalumu wa lugha za Kibantu wa kuzigawa nomino katika ngeli mbalimbali. Hivyo, kwa kuzingatia mfumo huu wa ngeli lugha ya Kiswahili ina ngeli 18 za nomino. Lakini lugha ya Kiarabu haifuati utaratibu huu wa kuzigawa nomino bali nomino zinaweza kuainishwa kwa kugaiwa makundi zaidi ya 50 (Muhammad, 2006).

Katika kigezo hiki cha mfumo wa ngeli lugha ya Kiswahili pia inatofautiana sana na lugha ya Kiarabu. Tofauti hizo zinajibainisha katika viambishi ngeli vya nomino, ujinsia unaojitokeza katika nomino za Kiarabu kwa kubeba viambishi vyenye kuonesha jinsia ya kike na maumbo hayo kufuata umoja na wingi. Katika sehemu ifuatayo tutaangalia viambishi ngeli, na ujinsia.

**Viambishi Ngeli**

Katika lugha ya Kiswahili nomino nyingi huanza na viambishi awali ngeli ambavyo huonesha umoja na wingi isipokuwa kwa baadhi ya nomino ambazo maumbo yake ya umoja na wingi ni yale yale. Kwa upande wa lugha ya Kiarabu maneno yake huwa na umoja, uwili na wingi. Tuchunguze mifano ifuatayo hapa chini:

13. **Kiswahili**

| **Umoja** | **Uwili** | **Wingi** |
|---|---|---|
| **mwa**limu | - | **wa**limu |
| **m**ti | - | **mi**ti |
| **ji**cho | - | **ma**cho |
| **ø**soko | - | **ma**soko |
| **ki**tabu | - | **vi**tabu |

Katika mifano (13) hapo juu tunabaini kuwa nomino za kiswahili huanza na viambishi ngeli vikifuatiwa na shina la neno. Pia, maumbo hayo ya nomino yana umoja na wingi tu. Lakini maneno hayohayo katika lugha ya Kiarabu hali ni tofauti na hiyo, kama tunavyoona katika mifano ifuatayo:

14.**Kiarabu**

| **Umoja** | **Uwili** | **Wingi** |
|---|---|---|
| Muʕalim | muʕalim**aan** | muʕalim**uwna** |
| shajarat | shajarat**aan** | ashjaarun |
| ʕayn | ʕayn**aan** | ʕuyuun |
| suwq | suwq**aan** | as’waaq |
| kitaab | kitaab**aan** | kutubu |

Katika mifano (14) hapo juu tunabaini kuwa viambishi vya umoja na wingi hukaa mwishoni mwa nomino, mfano, ‘kitaab**aan**’. Pia, maumbo hayo yana umoja, uwili na wingi (kitaabun>Kitaabaan>kutubu). Hali kadhalika baadhi ya nomino za lugha ya Kiarabu huvunjika umbo lake katika wingi, mfano, ʕayn>ʕaynaan>**ʕuyuun.**

**Ujinsia**

Aidha, nomino katika lugha ya Kiarabu zina viambishi ambavyo huonesha ujinsia ambapo katika Kiswahili hazina viambishi vinavyodhihirisha ujinsia katika maumbo yake. Tuangalie mifano ifuatayo:

15.

| Kiarabu | Kiswahili | Kiarabu | Kiswahili |
|---|---|---|---|
| muslim | ‘muislamu +me’ | muslam**at** | ‘muislamu +ke’ |
| mualim | ‘mwalimu +me’ | mualim**at** | ‘mwalamu +ke’ |
| twaalib | ‘mwanafunzi +me’ | twaalib**at** | ‘mwanafunzi +ke’ |

Katika mifano (15) tunaona kuwa maumbo ya nomino za lugha ya Kiarabu huongezewa kiambishi ‘**-at**’ kuonesha jinsia ya kike ambapo katika lugha ya Kiswahili nomino hazichukui viambishi kuonesha jinsia.

Zaidi ya hayo, msamiati mpya unaoingia katika lugha ya Kiswahili kutoka lugha ya Kiarabu na lugha nyingine yoyote sharti ufuate utaratibu wa Kiswahili (Chiraghdin na Mnyampala, 1977). Tuchunguze mifano ifuatayo:

16.

| Kutoka Kiarabu | | Kiswahili Umoja | Kiswahili Wingwi |
|---|---|---|---|
| muʕalim | > | **mw**alimu | **wa**limu |
| kitaab | > | **kit**abu | **vi**tabu |
| suwq | > | soko | **ma**soko |

Katika mifano (16) tunabaini kuwa nomino za Kiarabu zinapoingizwa katika lugha ya Kiswahili sharti zifuate utaratibu wa ngeli za Kiswahili. kwa mfano, neno **mw**alimu (umoja) na **wa**limu (wingi). Pia neno **ki**tabu (umoja) na **vi**tabu (wingi). Hii pia inatuthibitishia kiisimu lugha ya Kiswahili zinatofautiana sana na lugha ya Kiarabu.

**Hitimisho**

Kwa kuhitimisha makala haya tunaweza kusema kwamba kutokana na ulinganishi, mjadala na ushahidi uliotolewa iwe ni katika makala haya, au kwingineko hakuna ushahidi thabiti unaotumia vigezo madhubuti kuonesha kuwa Kiswahili asili yake ni kutokana na Kiarabu. Ushahidi wa kiisimu tuliouonesha katika makala haya unatudhihirishia wazi kuwa lugha hizi hazina asili wala mnasaba mmoja. Aidha, hatuwezi kuikataa fikra ya uwezekano wa watu wa mwambao huu kuingiliana na kuathiriana na wageni wa Kiarabu kiasi cha kuifanya lugha ya Kiswahili kupata athari kubwa kutoka lugha ya Kiarabu hususani katika msamiati. Hata hivyo, lugha haiwezi kupewa jina au kuingizwa katika kundi fulani la lugha kwa athari ya msamiati pekee. Tungeweza kuzinasibisha lugha hizi endapo zingefananafanana walau kwa kiasi fulani katika vipengele vya kifonolojia, mofolojia na mfumo wa ngeli za nomino. Kwa ujumla, uchunguzi huu wa kiisimu umeweza kuweka bayana lugha ya Kiswahili haitokani na lugha ya Kiarabu. Bila shaka, walioshikilia hoja hiyo walifanya hivyo kwa kutokuelewa ukweli wa mambo tu.

**Marejeo**

Akidah, M.A (2013). “Phonological and Semantic Change in Language Borrowing: The Case of Arabic words Borrowed into Kiswahili”. ktk *International Journal of Education and Research Vol. 1 No. 4 April 2013.*

Alidina, M. M. H. (1978). The Persian Factor in Kiswahili, *AFRICA EVENTS*, May 993: 30–31, London.

Allen, J. W. T. (1970). *The Swahili and Arabic Manuscripts in the Library of the University of Dar es Salaam: a Catalague,* Leiden.

Anttila, R. (1972). *An Introduction to Historical and Comparative Linguistics.* New York. Macmillan Publishing Co. Inc

Bosha, I. A. (1993). *Taathari za Kiarabu Katika Kiswahili, Kamusi Tathlitha Kiswahili Kiarabu na Kiingereza.* University of Dar es Salaam.

Chiraghdin, S na Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili,* Nairobi: Oxford University Press.

Freeman-Greenville, G.S.P. ( 1988). *The Swaahili Coast, 2nd to 19th Centuries*. London.

Krum, B. (1940) . *Words of Oriental Origin in Swahili*, The Sheldon Press, Northumberland Avenue W.C. 2

Lodhi, A. (2015). *Oriental Loanwords in Swahili.* Nairobi: Oford University Press.

Lodhi, A. Y. (2000). *Oriental loans in Swahili- A Study in Language and Culture Contacts*. Gothenburg.

Massamba, D. P. B. (2002). *Historia ya Kiswahili: 50BK hadi 1500BK.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Massamba, D. P. B. (2007). *Kiswahili Origins and The Bantu Divergence -Convergence Theory.* Dar es Salaam. TUKI: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Massamba, D. P. B., Kihore, Y. M. na Hokororo, J. I. (2001). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA); Secondari na Vyuo.* Dar es Salaam: TUKI. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Muhammad, M. E. (2006). *From the Treasures of Arabic Morphology.* Academy for Islamic Research Madrasah In'amiyyah: Camperdown

Mwita, C.M. (2009). "The Adaptation of Swahili Loanwords from Arabic: A Constraint Based Analysis", ktk *The Journal of Pan African Studies, Volume 2, number 8: 46-61*

Nurse, D. (1982). "The Swahili Dialects of Southern Somalia and the Southen Kenya Coast". ktk. M. P. Rumbi *The Bantu Original.* Uk.73-121, SELAF.

Reusch, R. (1953). "How the Swahili People and Language came to Existence", in *Tanganyika Notes and Records,* 34: 24

Steere, E. (1870). *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar.* London: Bell and Daldy.